



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Barua pepe: gdgeneral@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz
Simu ya Bure : 113

1 Mtaa wa TAKUKURU,
S. L. P 1291,
41101 DODOMA.

ONYO KWA MATAPELI KUHUSU AJIRA ZA TAKUKURU

Dar Es Salaam.
Februari 9, 2024

Ndugu Wanahabari;

Januari 31, 2024, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - TAKUKURU ilitoa tangazo la NAFASI ZA KAZI, kwa kada ya Afisa Uchunguzi nafasi 250 na kada ya Mchunguzi Msaidizi nafasi 100.

Pamoja na mambo mengine, tangazo hili limetamka bayana sifa za kitaaluma na vigezo ambavyo mwombaji anapaswa kuwa navyo ili kuwasilisha maombi yake na ilielezwa kwamba maombi ya nafasi hizo yanatakiwa kutumwa TAKUKURU kwa njia ya mfumo unaopatikana katika Tovuti ya TAKUKURU yenye anuani ya www.pccb.go.tz.

Hata hivyo, imebainika kwamba limeibuka wimbi la matapeli wanaowadanganya wananchi kwa kujifanya kuwa wao ni MAWAKALA na kudai kwamba wanaweza kuwasaidia kuwapatia nafasi za kazi ndani ya TAKUKURU.

Mfumo wa kuwasilisha maombi ya ajira TAKUKURU ni wa wazi na huru kwa Mtanzania yeyote aliyekidhi sifa na vigezo vilivyobainishwa na ifahamike kwamba maombi ya ajira yatakayowasilishwa kwa njia ya barua na kuifikisha ofisini au hata kwa kuituma kwa njia ya posta, hayatapokelewa.

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU



113/*113#



Takukuru Tz



[takukuru.tz](https://www.takukuru.tz)



TAKUKURU TV



[TAKUKURU.TZ](https://www.takukuru.tz)



Download on the App Store



GET IT ON Google Play

TAKUKURU APP 3.1

Tunarudia kuwaasa Wananchi, msidanganyike kwani hakuna wakala au mtu yeyote wa kati anayeweza kuwasaidia kwa lolote. Tunatoa rai kwa wazazi wenye watoto wenu, tafadhali wahimizeni vijana wenu kuwasilisha maombi yao TAKUKURU lakini kwa kufuata utaratibu tuliutangaza katika tangazo la ajira.

Kupitia taarifa hii, TUNATOA ONYO KALI KWA WOTE WANAOJIFANYA MAWAKALA WA KUWAPATIA WATU AJIRA ZA TAKUKURU. TUNATUMIA FURSA HII KUWAAMBIA MATAPELI HAO KUWA HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YAO PALE WATAKAPOBAINIKA KUENDELEA NA TABIA HIYO.

Tunaendelea kuukumbusha umma kuwa TAKUKURU ina ofisi katika kila Mikoa na katika wilaya zote Tanzania Bara. Hivyo, mtu yeyote akatakayebaini kuna mtu anataka kufanya utapeli, tafadhali atoe taarifa TAKUKURU au Kituo cha Polisi kulichoko karibu naye na iwapo upo kijijini basi unaweza pia kufika katika ofisi za Mtendaji wa Kata na kutoa taarifa hiyo. Kwa wenye simu za viganjani mnaweza kuwasiliana nasi BURE kupitia namba ya dharura 113.

"KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU"

Imetolewa na



Doreen J. Kapwani

MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI.

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU



113/113#



Takukuru Tz



takukuru.tz



TAKUKURU TV



TAKUKURU.TZ

Apple Store Google Play

TAKUKURU APP 3.1